Kujiandaa Kwa ajili Ya Kuja Kwake Kristo

(Preparing For Christ's Coming)

Na

Ellis P. Forsman

Kujiandaa Kwa ajili Ya Kuja Kwake Kristo

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 7, 2011

Kujiandaa Kwa ajili Ya Kuja Kwake Kristo

1 Wathesalonike 5:1-11

Je tumejiandaa kwa ajili ya kuja kwake Kristo? Je atatukuta tuko tayari atakapokuja? Tuwetayari tunapaswa kufa kabla hajaja?

Katika sura ya mwisho ya waraka wa Paulo kwa Wathesalonike, tunakuta akisema jinsi Wakristo wanavyopaswa "Kujiandaa Kwa ajili Ya Kuja Kwake Kristo"

1 Thes. 5:1-11, "*Lakini ndugu kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwizi ajavyo usiku. Wakati wasema kuna amani na salama ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa. Bali ninyi ndugu hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi. Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wa usiku, wala wa giza. Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Maana walalao usingizi hulala usiku pia na walewao hulewa usiku. Lakini sisi tulio wa mchana, tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo yetu iwe tumaini na wokovu. Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala. Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya.*"

Maandalizi thabiti ya kuja kwake Yesu hutupeleka kuhesabu kwamba…

Atakujaa Kama Mwivi Usiku (ms. 1-4)

Kwa baadhi, na siyo kwa wengine

Kuja kwake Bwana itakuwa mshangao kwa wengi, kama "*mwivi usiku*" inaonyesha wazi.

- 1 Thes. 5:2, "*Maana ninyi wenyewe mnajua ya kini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku.*"
- 2 Pet. 3:10, "*Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa msshindo mkuu na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.*"

Lakini kwa wale wanaotii maonyo ya Maandiko, “Siku” itawapita kama mwivi.

- 1 Thes. 5:1-2, “*Lakini ndugu kwa habari ya nyakati na majira, hamna haja niwaandikie. Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku.*”
- 1 Thes. 5:4, “*Bali ninyi ndugu hammo gizani, hata siku ile iwapate kama mwivi.*”

Kwa nini? Kwa sababu watakuwa tayari kwa kuja kwake, hataivyo hatujui itakuwa lini. Kwa sababu watakuwa wameweka moyoni maonyo ya kuzingatia kwa sasa.

Kwa wengine, yatakuwa ni maangamizi yasiyoepukika

Atakuja wakati watu wanasema “amani na usalama!”

1 Thes. 5:3, “*Wakati wasemapo kuna amani na usalama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa.*”

Siyo wakati wa shida, lakini katika nyakati za amani. Bado, Wakristo wengi wanadhani atakuja kukiwa na machafuko.

Atakapokuja, itakuwa na “maangamizi ya ghafla”.

1 Thes. 5:3, “*Wakati wasemapo kuna amani na usalama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla kama vile utungu umjiavyo mwenye mimba, wala hakika hawataokolewa.*”

Kama vile uchungu wa uzazi unavyokuja kwa mwanamke mwenye mimba. Hakutakuwa na wakati wala njia ya kukimbia uharibifu huu, ambayo inaelezwa kwa undani katika waraka wa pili wa Wathesalonike.

2 Thes. 1:7-10, “*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoangamizwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake; yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu.*”

“Siku” hii itakuwa moja ya utukufu kwa wale waliotayari.

2 Thes. 1:10, “*Yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake, na kustaajabiwa katika wote waliosadiki katika siku ile, kwa sababu ushuhuda wetu ulisadikiwa kwenu.*”

Kwa wale ambao sasa "wanalala ndani ya Yesu". 1 Thes. 4:13-16, "*Lakini ndugu hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na tumaini. Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza.*"

Kwa wale waliojiandaa kwa kuja kwake atakaposhuka. 1 Thes. 4:17-18, "*Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa na Bwana milele. Basi, farijianeni kwa maneno hayo.*"

"Siku" hii itamanisha nini kwetu, Bwana akija "*kama mwivi usiku*"? siku ya maangamizi au siku ya furaha? Inategemea kama iwapo tumejiandaa kwa kuja kwake, na maandalizi thabiti humanisha…

Tunapaswa Kuishi Kama Wana wa Mchana (ms. 5-11)

Kuwa macho na kutulia

Sisi ni "wana wa nuru" na "wana wa mchana". 1 Thes. 5:5, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa nuru, na wana wa mchana; sisi si wausiku wala wa giza.*"

Kwa sababu tunamfuata Yesu, "nuru ya ulimwengu".

- Yoh. 8:12, "*Basi Yesu akawaambia tena akasema, Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.*"
- Yoh. 12:35-36, "*Basi Yesu akawaambia, nuru ingaliko pamoja nanyi muda kidogo. Enendeni maadam mnayo nuru hiyo, giza lisije likawaweza; maana aendaye gizani hajui aendako. Maadamu mnayo nuru, iaminini nuru hiyo, ili mpate kuwa wana wa nuru. Hayo aliyasema Yesu akaenda zake, akajificha wasimwone.*"

Kwa sababu sasa tuko ndani ya Yesu, na kutembea nuruni.

Wakristo ni wana wa nuru.

- Efe. 5:8, "*Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru,*"

- 1 Yoh. 1:5-7, "*Na hii ndiyo habari tuliyoisikia kwake, na kuihubiri kwenu ya kwamba Mungu ni nuru, wala giza lo lote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiana naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli; bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.*"

Kwa sababu tumeacha matendo ya giza, na kutafuta kutembea vizuri.

- Rum. 13:11-14, "*Naam, tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana sasa wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini. Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia, basin a tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tama zake.*"

Tunapaswa kuwa macho wakati wa kuja kwake.

1 Thes. 5:6, "*Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi.*"

Maana hakuna ajuaye siku wala saa.

- 1 Thes. 5:2, "*Maana ninyi wenyewe mnajua yakini ya kuwa siku ya Bwana yaja kama vile mwivi ajavyo usiku.*"
- Mat. 24:36, "*Walakini habari ya siku ilke na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbingni, wala Mwana, ila Baba peke yake.*"
- Mat. 24:42, "*Kesheni basi kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu.*"

Kukesha hujumuisha sala. 1 Pet. 4:7, "*Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi iweni na akili mkeshe katika sala.*"

Kukesha hujuisha toba na kuimarisha tulichonacho. Ufu. 3:2-3, "*Uwe mwenye kukesha ukayaimarishe mambo yaliyosalia, yanayotaka kufa. Maana sikuona matendo yako kuwa yametimilika mbele za Mungu wangu. Basi kumbuka jinsi ulivyopokea, na jinsi ulivyosikia; yashike hayo na kutubu. Walakini usipokesha nitakuja kama mwivi, wala hutaijua saa nitakayokuja kwako.*"

Kwa upande mwingine, "lala" katika kifungu chetu cha maandiko inaongelea uzembe wa kiroho. 1 Thes. 5:6-7, "Basi tusilale usingizi kama

wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Maana walalao usingizi hulala usiku, pia na walewao hulewa usiku."

Tunapaswa kuwa na kiasi.

1 Thes. 5:6-8, "*Basi tusilale usingizi kama wengine, bali tukeshe na kuwa na kiasi. Maana walalao usingizi hulala usiku, pia na walewao hulewa usiku. Lakini sisi tulio wa mchana tuwe na kiasi, …*"

Neno "kiasi" inamanisha wastani au kujizuia, hasa katika swala la mvinyo. Hutumika zaidi katika hali ya ujumla kuwa na kiasi, kukesha.

Angalia jinsi Yesu anavyohusisha hii katika kukesha kwa ajili ya kuja kwake katika Luka 21:34-36, "*Basi jiangalieni mioyo yenu isije ikalemewa na ulafi, na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula kama mtego unasavyo; kwa kuwa ndivyo itakavyowajilia watu wote wakaao juu ya uso wa dunia nzima. Basi kesheni ninyi kila wakati, mkiomba ili mpate kuokoka katika haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa Adamu.*"

Tunapaswa kwa hakika kuchukua ahadi ya kuja kwa Yesu tukimanisha, siyo kizembe.

Kuvaa silaha na kusubiri

Katika kiasi chote (kumaanisha), vaa "silaha za Mungu). 1 Thes. 5:8, "*Lakini sisi tulio wa mchana tuwe na kiasi, hali tukijivika kifuani imani na upendo, na chapeo yetu iwe tumaini la wokovu.*"

Kama vile chapeo ya tumaini na upendo.

Imani na upendo hukinga mioyo yetu kuepukana na uovu mwingi. Imani huja kutoka katika neno la Mungu, na upendo utoka kwake yeye ambaye ndiye Neno.

- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"
- 1 Yoh. 3:16, "*Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.*"

Kama vile ilivyo tumaini la wokovu kama dirii.

Tumaini la wokovu wetu hukinga nia zetu katika uoga na mashaka. Tumaini pia hutoka katika neno la Mungu.

- Rum. 15:4, "*Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.*"

- Efe. 6: 11-18, "*Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzishinda hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali juu ya falme na mamlaka; juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu war oho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi siamameni hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga war oho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote;*"

Ametuhimiza kusubiri kwa sababu Mungu ametuchagua katika wokovu.

1 Thes. 5:9-10, "*Kwa kuwa Mungu hakutuweka kwa hasira yake, bali tupate wokovu kwa Bwana wetu Yesu Kristo; ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala.*"

Hakutuchagua katika hasira. Siku ya hasira yaja.

Rum. 2:4-11, "*Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake, na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? Bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu, atakayemlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake; wale ambao kwa sababuri katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele; na wale wenye fitina wasioitii kweli, bali wakubalio dhuluma watapata hasira na ghadhabu;dhiki na shida juu ya kila nafsi ya mwanadamu atendaye uovu, Myahudi kwanza na Myunani pia; kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu.*"

Alafu, Yesu amekuja kututoa kwenye ghadhabu. 1 Thes. 1:10, "*Na kumngojea Mwanawe kutoka mbinguni, ambaye alimfufua katika wafu, naye ni Yesu mwenye kutuokoa na ghadhabu itakayokuja.*"

Ametuchagua katika wokovu kupitia damu ya Mwanawe.

Rum. 5:8-10, "*Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa kwa ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa*

tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake."

Sasa ikiwa "tumeamka au tumelala" (kufa au kuishi), tunaishi pamoja na Kristo!

- 1 Thes. 4:14, "*Maana ikiwa twaamini kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.*"
- 1 Thes. 4:17, "*Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa na Bwana milele.*"
- Fil. 1:21-23, "*Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo na kufa ni faida. Ila ikiwa kuishi katika mwili kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi nitakalolitachagua silitambui. Ninasongwa katikati ya mambo mawili; ninatamani kwenda zangu nikae na Kristo maana ni vizuri zaidi sana;*"

Farijiwa na kuimizwa

Tunatakiwa kufarijiana.

1 Thes. 5:11, "*Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya.*"

Kwa faraja kila mmoja anapokea kutoka kwa Mungu. 2 Kor. 1:3-4, "*Na ahimidiwe Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili tupate kuwafiriji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo tuanazo farijiwa na Mungu.*"

Kwa faraja ya tumaini letu tulionayo katika Kristo. 1 Thes. 4:18, "*Basi farijianeni kwa maneno hayo.*"

Tunapaswa kuhimizana (kujenga) mmoja baada ya mwingine.

1 Thes. 5:11, "*Basi farijianeni na kujengana kila mtu na mwenzake, vile vile kama mnavyofanya.*"

Lengo tunalopaswa kuwa nalo.

- Rum. 14:19, "*Basi kama ni hivyo, na mfuate mambo ya amani na mambo yafaayo kwa kujengana.*"
- Rum. 15:2, "*Kila mtu miongoni mwetu na ampendeze jirani yake, apate wema akajengwe.*"

Kazi ya msingi ya kanisa ni kuelimisha.

- Efe. 4:11-12, "*Naye alitoa wengine kuwa mitume na wengine kuwa manabii na wengine kuwa wainjilist na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe.*"
- Efe. 4:15-16, "*Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*"

Hitimisho

Je tunapaswa kuwa tayari Kristo akija? Yote inategemea…

- Je tunakesha? Je tunatilia maanani kuhusu kuja kwake?
- Je tunavaa silaha za Mungu? Kwa imani na upendo kama chapeo inayokinga roho zetu? Kwa taraja la wokovu kama dirii ya kukinga nia zetu?
- Je tumejiingiza katika kuwafariji na kuwa elimisha wengine?
- Kama ndivyo, hakika sisi ni "wana wa nuru na wana wa mchana"!

Kumbuka kilicho muhimu kwetu sisi kufanya mambo haya

- Neno la Mungu linalojenga imani na tumaini; ambayo pia hutoa faraja.
- Kanisa la Kristo ambapo upendo unapaswa kuonyeshwa miongoni mwa waumini; sehemu ambapo faraja na elimu inapaswa kuonyeshwa na waumini.

"Kujiandaa Kwa ajili Ya Kuja Kwake Kristo" haitokei bila kulitumia Neno la Mungu na kushiriki katika utendaji kazi katika kanisa la Bwana.

Je umezidishwa na Bwana katika kanisa lake?

- Mdo. 2:41, "*Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.*"
- Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Mtu anazidishwaje ndani ya kanisa? Mtu lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Matend 11:18, "...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye.*" (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "Kwa ajili ya ondoleo la dhambi". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo

ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi “kunyunyiza”. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika mshiriki wa kundi la Mkristo, kwa nini usifanyike leo?